# pspptb na matukio

Dodoma - Tanzania

Toleo Na 02-Julai - Disemba 2025


# Wanataaluma wa ununuzi na ugavi waliosajiliwa kuimarisha ukaguzi





## PSPTB yang'ara tuzo taasisi za serikali

Uk. 6



## PSPTB yaimarisha taaluma kwa wanafunzi

Uk. 8

Scan Me

# Karibu Katika Toleo la Pili la Jarida la PSPTB

Ndugu Msomaji, Napenda kutambulisha katika toleo jipya kabisa la Habari na kukuhabarisha katika toleo jipya la jarida la PSPTB.

PSPTB inayofuraha kukuletea chapisho ambalo lina lengo la kuhabarisha, kuhamasisha na kushirikisha umma katika kutekeleza majukumu yake katika kusimamia Ununuzi na ugavi nchini Ni wajibu wetu kuufahamisha umma juu ya mipango yetu, mikakati yetu na maendeleo ya utekelezaji wa kazi zetu katika kufikia malengo tuliyojiwekea kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi.

Katika kufikia malengo yetu, tutahakikisha tunaujulisha umma Pamoja na wadau kwa ujumla juu ya changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa majukumu yetu ili kujenga uelewa wa Pamoja na hivyo kurahisisha utatuzi wa changamoto hizo.

Jarida hili ni kwa ajili ya umma wa Watanzania na wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi kujifunza na kutambua uwepo wa PSPTB kama Chombo kinachoweza kuangazia fursa zilizopo au zinazoweza kujitokeza kwaajili ya maendeleo ya kibiashara, changamoto za ununuzi na ugavi kukiwa na lengo la Pamoja la kujenga Uchumi imara wa nchi yetu.

Kupitia jarida hili tutaunganisha sauti za wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi, watunga sera na watoa maamuzi Pamoja na walaji wa mwisho ambao ndio wanatoa mchango mkubwa katika ununuzi na ugavi hivyo kukuza Uchumi wetu.

Jarida hili linachapishwa mara mbili kwa mwaka na linatumika kama kipaza sauti au jukwaa la usambazaji wa taarifa zinazohusu ununuzi na ugavi katika kupanua wigo wa uelewa kwa wadau na umma kwa ujumla.

Jarida hili pia linatarajiwa kuongeza thamani kwa shughuli za PSPTB kwa kujenga mawasiliano ya karibu na wadau waliopo na kuwavuta wapya kwenye mnyororo wa sekta ya ununuzi na ugavi ndani na njee ya nchi.

Malengo mengine ya jarida hili yatakuwa kuzijulisha sekta zingine za Uchumi kuhusu shughuli za PSPTB, kuwa jukwaa la kubadirishana Mawazo kwaajili ya kukuza sekta ya ununuzi na ugavi Pamoja na kutoa Habari sahihi kuhusu nafasi ya PSPTB katika kuikuza sekta hii muhimu

Tunatarajia kwamba wadau wa sekta bya ununuzi na ugavi Pamoja na wasomaji wote watakaofikiwa watatupa mrejesho utakaosaidia kuboresha jarida hili kwa manufaa ya maendeleo ya taifa katika kulinda maslahi ya nchi Pamoja



**CPSP Godfred Mbanyi**
**Mkurugenzi Mtendaji**





## Bodi ya Uhariri

**Bi Shamim Mdee**
Mwenyekiti

**Bi Beatrice Sanga**
Katibu

**Bi Ikunda Erick**
Mhariri

**Dickson Mollel**
Mwandishi

**Wakili Hamza Twaha**
Mjumbe

**Boniface Mushi**
Mjumbe




# Wanataaluma wa Ununuzi na Ugavi waliosajiliwa kuimarisha ukaguzi

**Imeelezwa kuwa uwepo wa wataalamu wa manunuzi na ugavi waliopatiwa mafunzo ya ziada na kusajiliwa na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) utasaidia kwa kiwango kikubwa kuimarisha tasnia ya ukaguzi wa mnyororo wa ugavi nchini.**

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bi Jenifa Omolo, wakati akihutubia mahafali ya 14 ya PSPTB, yaliyofanyika Oktoba 24, katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Bi Omolo amesema hatua hiyo itaiwezesha PSPTB kuongeza tija katika ukaguzi, kubaini kasoro zinazojitokeza na kuweka mikakati ya kuzirekebisha ili kufanya mfumo wa ugavi kuwa imara, wenye uwazi na ufanisi zaidi.

"Natoa rai kwa makampuni ya ukaguzi kuona umuhimu wa kuwaajiri wataalamu wa manunuzi na ugavi ili kusaidia katika utekelezaji wa majukumu yao ya ukaguzi. Kwa muda sasa kuna baadhi ya waajiri wanafumbia macho mchango wa fani hii," amesema Bi Omolo.

Aidha, amewataka wahitimu wa PSPTB kufanya kazi zao kwa uadilifu, weledi na uaminifu, akisisitiza utekelezaji wa majukumu ya ununuzi na ugavi bila taaluma ni ukiukwaji wa Sheria ya PSPTB Na. 23 ya mwaka 2007.

Katika hotuba yake, Bi Omolo ameelekeza waajiri wote wa sekta ya umma na binafsi kuzingatia matakwa ya kifungu cha 11 cha sheria hiyo,kinaweka adhabu kwa wote watakaobainika kukiuka masharti yake.

Pia ameagiza bodi hiyo kuendelea kusimamia utekelezaji wa sheria kwa kufanya ukaguzi wa kina katika taasisi zote za umma na binafsi.

"Tutalitazama hili kwa makini. Bila kufaulu mitihani ya bodi, huwezi kupanda cheo. Zamani bila kuwa na CPA huwezi kuwa mhasibu; vivyo hivyo, bila taaluma hii huwezi kuwa Afisa Manunuzi," amesisitiza Bi Omolo.



Aidha ameagiza bodi hiyo kupitia Kamishna wa Sera na Ununuzi katika Wizara ya Fedha, kuhakikisha maslahi ya wataalamu wa kada ya ununuzi na ugavi yanashughulikiwa ipasavyo.

Bi Omolo pia amekumbusha wakurugenzi, wakuu wa idara na wataalamu wa vitengo vya ununuzi na ugavi kuhakikisha wana sifa zinazotambulika kisheria kwa mujibu wa Sheria ya PSPTB ya mwaka 2007 na Waraka wa Hazina Na. 3 wa mwaka 2015.

Mwenyekiti wa Bodi ya PSPTB, Bw Jacob Kibona, ameiishukuru serikali kupitia wizara ya fedha kwa kuipatia bodi hiyo Sh milioni 900 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake, zikiwemo shughuli za ukaguzi katika zaidi ya taasisi 300 za serikali.

Aidha, amemuomba mgeni rasmi kusaidia upatikanaji wa ofisi rasmi ya PSPTB, ombi ambalo Naibu Katibu Mkuu alilikubali na kuahidi kulifanyia kazi haraka.

Kwa upande mwingine, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Profesa Elisante Ole Gabriel, ameahimiza wahitimu wa PSPTB kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu, akisema mafanikio ya taaluma hayatategemea vyeti walivyopata, bali namna watakavyovitumia kwa matendo mema.

"Vyeti havitakuwa na maana kama vitatumika kinyume na maadili ya taaluma. Mafanikio yatatokana na uaminifu, uwajibikaji na kufanya kazi kwa moyo wa uzalendo," amesema Profesa Ole Gabriel.

Mahafali hayo yaliambatana na utoaji wa vyeti kwa wahitimu wa mitihani ya kitaaluma ya PSPTB, na yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wakufunzi, wadau wa sekta ya manunuzi na ugavi, pamoja na familia za wahitimu.




# Wataalamu wa ununuzi na ugavi watakiwa kuzingatia weledi

**WAHITIMU wa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) wametakiwa kutumia taaluma yao na kufanya manunuzi kwa kuzingatia weledi, uaminifu na maadili kwani utalitendea taifa haki na kuleta maendeleo.**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo alieleza hayo jijini Dar es salaam katika mahafali yaliyohusisha wahitimu 368 wa bodi hiyo wakiwemo wataalam wa ngazi ya stashahada, shahada ya kwanza na shahada ya juu ya kitaaluma ya un unuzi na ugavi

Omolo alisema ikiwa wanataaluma watatumia taaluma yao kufanya manunuzi ya kitaalam kwa weledi na kutendea haki maeneo hayo mawili kwa moyo, uaminifu na maadili watatendea taifa haki kwa kuleta maendeleo.

Alisema kwa upande wa serikali na walezi wa kada hiyo wanachukulia suala la weledi kwa uzito kwani limekuwa changamoto kubwa kwenye sekta hiyo ya ununuzi na ugavi.

"Nina Imani wahitimu wa shahada ya juu ya kitaaluma ya ujuzi na ugavi mtaonesha uzalendo na utayari wenu katika kutumikia taaluma na nchi yetu kwa uadilifu na weledi, mwenyezi Mungu awasimamie muweze kutumia viapo mtakavyoapa. amesema Omolo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya PSPTB, Jacob Kibona amesema bodi hiyo imekuwa ikifanya ushirikishwaji wa wadau katika utendaji kazi wake na kwa jitihada na weledi wao wamekuwa na mchango mkubwa katika kuwapata wahitimu hao na waliotangulia.

Naye mmoja wa wahitimu wa masomo ya CPSP, Dominick Abdalah amesema wamejipanga kusaidia taasisi wanazofanyia kazi na jamii kuhakikisha wanafanya manunuzi kwa kuzingatia ubora ili fedha za serikali katika miradi ikidhi viwango na thamani inayowekwa.





*Watahiniwa wa mitihani ya PSPTB katika chumba cha mitihani wakati wa mitihani hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa Suma JKT Jijini Dar es Salaam*

# PSPTB yatangaza matokeo ya mitihani ya bodi, yaonya kuhusu udanganyifu

**BODI ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), imetangaza matokeo ya mitihani ya 31 ya bodi hiyo yanayoonesha jumla ya watahiniwa 186 kati ya 382 waliofanya mitihani hiyo wamefaulu sawa na asilimia 50.3.**

Mkurugenzi Mkuu wa PSPTB, Godfred Mbanyi, ametangaza matokeo ya hayo na kusema kati ya walioshiriki, 192 (sawa na 50.3%) wamefaulu, 186 (sawa na 48.7%) wamerudia masomo na watahiniwa wanne wamefeli na kulazimika kuanza upya katika ngazi husika.

Aidha, ametoa wito kwa watahiniwa waliokosa alama za kutosha kuwawezesha kufaulu wajisajili ili kurudia masomo kwenye mitihani ya Novemba mwaka huu 2025.

> "Wale waliokosa alama za kutosha dirisha la usajili la Novemba 2025 limefunguliwa, tunawahimiza wanafunzi waliomaliza vyuo kujisajili ili kupata sifa stahiki za kitaaluma

Mbanyi amesema dirisha la usajili limefunguliwa na kuwataka wanafunzi waliomaliza vyuo kujisajili kwa ajili ya kufanya mitihani hiyo ya kitaaluma ili waweze kupata sifa stahiki za kitaaluma.

"Wale waliokosa alama za kutosha dirisha la usajili la Novemba 2025 limefunguliwa, tunawahimiza wanafunzi waliomaliza vyuo kujisajili ili kupata sifa stahiki za kitaaluma" amesema, Mbanyi.

"Sambamba na hilo, amewaonya watahiniwa kuepuka vitendo vya udanganyifu na ukiukwaji wa kanuni za mitihani, akisisitiza kuwa bodi haitasita kuchukua hatua kali kwa yeyote atakayebainika kufanya udanganyifu.

Amesema adhabu kwa watakaobaikina kufanya udanganyifu kwa mujibu wa kanuni ni pamoja na kufutiwa matokeo ya mitihani yote, kusimamishwa mihula mitatu ya mitihani na kupewa adhabu ya kulipa fedha au kifungo jela.

"Bodi haitasita kuchukua hatua kali zaidi kwa yeyote atakayekiuka maadili ya mitihani, tunahitaji taaluma hii kuheshimika na kuaminika nkwa maslahi ya taifa", amesema Mbanyi.

# PSPTB yang'ara tuzo taasisi za serikali

**BODI ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), imepata tuzo ya mshindi wa pili katika Kundi la Taasisi za Serikali zilizoshiriki Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (DITF).**

Ushindi huo ni kutambua mchango wa bodi hiyo katika kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa weledi na ubunifu mkubwa.

Akizungumza mara baada ya kupokea tuzo hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano wa PSPTB,Shamim Mdee, alisema ushindi huo umetokana na maandalizi ya kina yaliyolenga kutoa huduma bora na zenye tija kwa wageni waliotembelea banda la PSPTB wakati wa maonesho hayo.

"Siri ya mafanikio haya ni maandalizi mazuri na timu yenye ari kubwa ya kuhakikisha kila mgeni anapata huduma bora. Tulihakikisha tunawasikiliza wageni kwa makini, kujibu maswali yao kwa kina na kuwaeleza kwa ufasaha huduma na bidhaa tunazotoa," amesema Mdee.

Ameongeza kuwa nidhamu ya utumishi wa umma, ubunifu wa banda,




na mwonekano wa kuvutia vilichangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha ushindi huo.

"Banda letu lilikuwa la kipekee kwa sababu tuliweka mkazo katika ubunifu, tulionyesha namna rahisi ya kupata huduma zetu kupitia mfumo wa mtandao wa Online Registration System, jambo lililowavutia wageni wengi," amefafanua.

Mdee amesema ushindani katika kundi la taasisi za serikali ulikuwa mkubwa kutokana na idadi ya taasisi zilizoshiriki, lakini mafanikio hayo ni matokeo ya ushirikiano mzuri na ufanisi wa timu nzima ya PSPTB iliyoshiriki kutoa huduma katika maonesho hayo.

Aidha, ameahidi kuwa PSPTB itaendelea kuboresha huduma zake kwa wadau wa taaluma ya ununuzi na ugavi nchini, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa dhamira ya bodi hiyo katika kukuza weledi, uwajibikaji na ubunifu katika sekta hiyo muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) ni chombo cha kitaifa kinachohusika na kusimamia taaluma ya ununuzi na ugavi nchini.

Baadhi ya majukumu yake ni pamoja na kuendesha mafunzo na mitihani ya kitaaluma, kusajili na kusimamia mienendo na maadili ya wataalam wa ununuzi na ugavi, pamoja na kutoa ushauri kwa serikali na sekta binafsi kuhusu masuala ya kitaaluma katika sekta hiyo.

Tuzo hiyo inaonesha jinsi PSPTB inavyoendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuimarisha taswira chanya ya taasisi hiyo katika kukuza taaluma ya ununuzi na ugavi nchini.





*Baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB kwenye picha ya pamoja walipotembelea banda la PSPTB wakati wa maonesho ya 49 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba)*

# PSPTB yapongezwa utoaji huduma maonesho ya DITF

**BODI ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) imepongezwa kwa utoaji bora wa huduma kwa umma katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) kwa kuhudumia wadau zaidi ya 495.**

Pongezi hizo ni baada ya kuibuka mshindi wa pili katika kipengele cha Taasisi Bora ya Serikali katika Utoaji Huduma Bora wakati wa Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), maarufu kama Sabasaba, yaliyofanyika Juni 28 hadi Julai 13, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano wa PSPTB, Bi Shamim Mdee, amesema lengo kuu la ushiriki wa bodi hiyo katika maonesho hayo lilikuwa ni kutoa elimu na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu majukumu na huduma zinazotolewa na PSPTB.

"Tulishiriki Sabasaba kwa dhamira ya kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yetu, hususan huduma zinazopatikana kupitia mfumo wa mtandaoni (ORS) kama vile usajili wa mafunzo na mitihani, usajili wa wanachama wa kitaaluma, watoa mafunzo, na kampuni za ushauri," amesema Mdee.

Ameongeza katika maonesho hayo, yalikuwa pia ni fursa ya kutoa msaada wa moja kwa moja kwa wadau waliokutana na changamoto ya kupata namba za malipo, usajili wa mitihani, uanachama, ushiriki wa matukio ya PSPTB, pamoja na kufanya masasisho ya taarifa binafsi katika akaunti zao.

Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana wakati wa maonesho hayo, Mdee amesema zaidi ya wadau 495 walitembelea banda la PSPTB na kuhudumiwa kulingana na mahitaji yao.

"Kati ya wageni hao, takribani 50 walikuwa na changamoto za usajili wa uanachama na kupata namba za malipo. Kufikia Julai 17, baadhi yao walikuwa tayari wamelipa ada za usajili na ada za uanachama wa mwaka," amesema Mdee.

Shamim ameongeza kuwa ushindi wa nafasi ya pili katika utoaji huduma bora ni ishara ya kutambua juhudi za bodi hiyo katika kuboresha huduma kwa umma kwa kutumia teknolojia, ubunifu na mawasiliano yenye tija.

Amesema PSPTB ilitumia maonesho hayo kujitangaza na kushirikiana na vyombo mbalimbali vya habari ili kuelimisha wananchi kuhusu shughuli zake na mafanikio yaliyopatikana.

Aidha alisema walitumia jukwaa hilo kuzindua Mitihani ya Kati ya Mwaka (Mid-Session Examination) na toleo la kwanza la Jarida la PSPTB 'PSPTB NA MATUKIO.'

Miongoni mwa vyombo vya habari vilivyoshirikiana na PSPTB ni TBC1, TBC2, Star TV, Channel Ten, EFM Radio, Michuzi Blog, Fullshangwe Blog, Daily News, HabariLEO, Dailynews Digital, Taifa Tanzania, UBX Media na PSPTB TV.

Shamim amehitimisha kwa kusema PSPTB itaendelea kutoa huduma bora zenye viwango vya juu na kuhakikisha kila mdau wa sekta ya ununuzi na ugavi anapata elimu, huduma na taarifa sahihi kwa urahisi kupitia mifumo ya kisasa ya kidijiti.

# PSPTB yaimarisha taaluma kwa kuwajengea uwezo wanafunzi wake

**BODI ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) imeendelea kuimarisha taaluma ya ununuzi na ugavi nchini kwa kutoa mafunzo maalum ya utafiti kwa wanafunzi na watahiniwa wa mitihani ya PSPTB.**

Wanafunzi hao ni miongoni mwa wale wa Certified Procurement and Supplies Professional (CPSP) wanaotarajia kuanza kufanya tafiti zao za kitaaluma.

Mafunzo hayo ya siku tano yamefanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango, Dodoma, yakihudhuriwa na zaidi ya wanafunzi 232 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kufanya tafiti bora na zenye viwango vya juu katika taaluma ya ununuzi na ugavi.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB, Godfred Mbanyi, amesema mafunzo hayo ni sehemu muhimu ya maandalizi kwa wanafunzi wa CPSP wanaokamilisha shahada zao za juu katika taaluma hiyo.

"Tumeendesha mafunzo ya siku tano ya maandalizi ya kufanya tafiti, kama hitaji maalum la kukamilisha shahada ya juu ya taaluma ya Ununuzi na Ugavi (CPSP)kwa wanafunzi wetu", amesema Mbanyi.

Amesema, wanafunzi hao wamepata nafasi ya kuelekezwa jinsi ya kufanya tafiti, kukusanya taarifa, na kufuata taratibu sahihi za kitaaluma lakini pia wamesisitizwa kujiepusha na kunakili kazi za wengine na badala yake wafanye tafiti zenye ubunifu, uaminifu na maadili," amesisitiza Mbanyi.




*Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB Ndg.Godfred Mbanyi akizungumza na Watahiniwa wa mitihani ya PSPTB wanaotarajia kufanya tafiti, wakati wa mafunzo ya namna ya kufanya tafiti (Research Methodology) katika Ununuzi na Ugavi yaliyofanyika katika ukumbi wa chuo cha mipango mkani Dodoma.*



*Watahiniwa wa mitihani ya PSPTB wanaotarajia kufanya tafiti wakiwa kwenye mafunzo ya namna ya kufanya tafiti (Research Methodology) katika Ununuzi na Ugavi yaliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Mipango mkoani Dodoma.*

Aidha, ameongeza kuwa PSPTB inaendelea kuhimiza vijana kuwa wazalendo, wabunifu, na wenye kujituma katika majukumu yao ya kila siku na kuepuka vitendo vya rushwa, ufisadi na mienendo isiyofaa inayoweza kuathiri taaluma na taifa kwa ujumla.

"Ni wajibu wa kila kijana anayeingia kwenye taaluma hii kuwa mfano wa uadilifu, uwajibikaji na uzalendo. Tunataka wataalamu wa ununuzi na ugavi watakaojivunia taaluma yao na kuilinda kwa kufanya kazi kwa weledi na maadili," amesisitiza Mbanyi.

Kwa upande wake, Felista Benjamin, mwanafunzi kutoka Mkoa wa Mwanza aliyeshiriki mafunzo hayo, amesema elimu aliyoipata itamsaidia katika maandalizi ya tafiti zake na kumjengea uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi.

"Mafunzo haya yamenisaidia kuelewa namna bora ya kufanya tafiti, jinsi ya kukusanya na kuchambua taarifa kwa usahihi, na kuepuka makosa ya kitaaluma,amebainisha Benjamin

Mafunzo hayo ya Research Methodology yamefanywa Julai 28 hadi Agosti Mosi 2025, yakilenga kuwajengea uwezo wanafunzi wa CPSP katika kufanya tafiti zenye tija na ubunifu.

Hii ni sehemu ya mkakati wa PSPTB wa kuendeleza weledi, kuimarisha ubora wa taaluma na kuhakikisha wataalamu wa ununuzi na ugavi nchini wanakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.



*Wajumbe wa baraza la wafanyakazi wa PSPTB kwenye picha ya pamoja mara baada ya ufunguzi wa kikao cha baraza hilo kilichofanyika katika Ukumbi wa ERB mkoani Morogoro tarehe 25, Septemba 2025*

# PSPTB yajipanga kuboresha utendaji 2025/2026

**BODI ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi nchini (PSPTB) imeweka mikakati mipya ya kuboresha utendaji wake kwa mwaka wa fedha 2025/2026, baada ya kufanya tathmini ya bajeti na mafanikio ya mwaka uliopita.**

Lengo la kimakati hiyo ni kuongeza ufanisi katika sekta ya ununuzi na ugavi.

Hayo yalibainishwa na Mkurgenzi Mtendaji wa PSPTB, Bw Godfred Mbanyi wakati akizungumza kwenye kikao kazi cha baraza la wafanyakazi wa bodi hiyo kilichofanyika mkoani Morogoro.

Amesema kikao hicho kimekuwa fursa ya kupitia malengo ya mwaka uliotangulia na kupanga hatua za kufanikisha mipango ya mwaka ujao.

"Kikao hiki kinatupatia nafasi ya kuangalia tulipanga kufanya nini mwaka uliopita, kuona ni yapi tumetekeleza, ni yapi tumeshindwa na changamoto tulizokutana nazo.," amesema Bw Mbanyi.

Amesema hatua hiyo itatusaidia kuweka mikakati mipya ya kuboresha utendaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

> "Bodi yetu inaendesha mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu wa vyuo vikuu wa ununuzi na ugavi. Mitihani hii huwapa nafasi ya kupata vyeti vya kitaaluma vinavyowawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na weledi...

Aidha, Bw Mbanyi amebainisha kuwa mageuzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) yamekuwa chachu ya kurahisisha mchakato wa usajili na mitihani ya kitaaluma, tofauti na awali.

Amesema awali kulikuwa na urasimu ambao bodi hiyo imefanikiwa kusajili zaidi ya wataalam 10,000 huku mwaka 2024 jumla ya wanafunzi 680 walifanyiwa mitihani ya kitaaluma ikilinganishwa na lengo la wanafunzi 750.

"Bodi yetu inaendesha mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu wa vyuo vikuu wa ununuzi na ugavi. Mitihani hii huwapa nafasi ya kupata vyeti vya kitaaluma vinavyowawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na weledi katika taaluma hii," ameongeza Bw. Mbanyi.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE)Tawi la PSPTB, Bi Faraja Mgulambwa, amesema kikao hicho ni jukwaa muhimu kwa wafanyakazi.

Amesema kikao hicho kinawawezesha kutoa maoni yao, kushirikiana na menejimenti, na kutafuta suluhu za changamoto zinazowakabili.

"Tumekutana hapa kwa siku mbili katika kikao kazi kinachotupa mwanga wa kujadili mambo mbalimbali ya taasisi yetu na kutafuta suluhu za changamoto za kazi," amesema Bi Mgulambwa.



*Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya PSPTB wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya mafunzo ya Uongozi na Utawala yaliyofanyika jijini Dar es salaam*



*Katibu Mtendaji wa Ozone International Bi. Khadija Masoud akichangia mada wakati wa mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo wadau wa mnyororo wa Ugavi kutoka taasisi mbalimbali Zanzibar, mafunzo hayo yaliandaliwa na ZPPRA Kwa kushirikiana na PSPTB.*



*Menejimenti ya mfuko wa taifa wa bima ya afya (NHIF) wakiwa katika picha ya pamoja na mkufunzi bi. Moza Hamisi mara baada ya mafunzo yaliofanyika jijini Arusha.*

# Uendeshaji wa Mitihani ya 31 ya PSPTB

**Bodi katika kutekeleza majukumu yake kupitia kifungu cha 7 (e) na (f) cha Sheria ya PSPTB No. 23 ya mwaka 2007 imeendesha mitihani ya ziada (Midsession Examinations) ya Taaluma ya Ununuzi na Ugavi nchini kuanzia tarehe 25.08.2025 mpaka tarehe 29.08.2025 katika Chuo Cha Mipango (IRDP) - Dodoma.**

Jumla ya watahiniwa 416 sawa na asilimia 83.2% walidahiliwa kati ya lengo la kudahili watahiniwa 500 ili kufanya mitihani hii kuanzia ngazi ya stashahada ya taaluma ya ununuzi na ugavi mpaka hatua ya utafiti (research). Kati ya watahiniwa waliodahiliwa, watahiniwa 382 sawa na 91.8% walifanya mitihani hii wakati watahiniwa 34 (8.2%) hawakuweza kufanya mitihani husika kwa sababu mbalimbali. Matokeo ya mitihani hii yanaonyesha watahiniwa 192 (50.3%) kati ya watahiniwa 382 walifaulu mitihani hii, watahiniwa 190 (48.7%) wanarudia masomo yao, na watahiniwa 4 (1.0%) walifeli.

Mafanikio makubwa ya mitihani hii ni pamoja na kuwezesha jumla ya watahiniwa 69 kushiriki katika mahafali baada ya kufanikiwa kufaulu mitihani yao. Mitihani hii imetoa fursa ya watahiniwa kupata sifa za kupandishwa madaraja, mishahara na kadhalika. Mitihani mingine ya PSPTB imepangwa kufanyika kuaniza tarehe 01 mpaka 05 Disemba 2025 katika vituo saba vilivyoko katika mikoa ya Dar Es Salaam, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Mbeya na Zanzibar.

Mahafali ya 14 ya PSPTB

Bodi iliendesha mahafali ya 14 ya wahitimu wa mitihani ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi yalijumuisha wahitimu wa Cheti cha Diploma ya Taaluma ya Ununuzi na Ugavi, Shahada ya taaluma ya Ununuzi na Ugavi na Shahada ya juu ya Ununuzi na Ugavi na Wahitimu wa Kozi maalum ya Ukaguzi wa Mnyororo wa Ununuzi na Ugavi ambao jumla yake ni wahitimu 499 – Jedwali 1.

Mahafali haya yalifanyika tarehe 25 Oktoba 2025 katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) jijini Dar es Salaam na Mgeni rasmi alikuwa Dkt. Natu El-maamry Mwamba - Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Katika mahafali haya jumla ya wahitimu 133 walitunukiwa vyeti vya Certified Procurement and Supply Auditors – CPSA wakiwa ni wahitimu wa kwanza wa kozi ya ukaguzi wa mnyororo wa ununuzi na ugavi.

Mafunzo mengine ya kozi ya wataalamu wa ukaguzi wa mnyororo wa ununuzi na ugavi yamepangwa kufanyika kuanzia tarehe 17.11.2025 mpaka 02.12.2025 kwa kozi ya muda mrefu na mafunzo mengine yatafanyika kuanzia tarehe 04.01.2026 mpaka tarehe 15.02.2026. Mafunzo haya yanajenga weledi na uelewa mkubwa kwa wataalam hawa na kwamba kwa kushirikiana na mamlaka zingine nchini, uwepo wao utasaidia sana utendaji na ufanisi wasekta ya Ukaguzi na hususani eneo la Ununuzi na Ugavi.



*Bw. Amani Ngonyani, Mkurugenzi wa Mitihani na Mafunzo ya Kitaalam*

| Aina ya Cheti | Novemba 2024 | Mei 2025 | Agosti 2025 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Cheti cha kitaaluma cha stashahada ya Ununuzi na Ugavi | 11 | 06 | 03 | 20 |
| Cheti cha Wahitimu wa Kitaaluma ya Ununuzi na Ugavi | 18 | 09 | 17 | 44 |
| CPSP | 129 | 126 | 49 | 304 |
| CPSA | 57 | 74 | - | 131 |
| **JUMLA** | **215** | **215** | **69** | **499** |



# Umuhimu wa Uelimishaji wa Umma Kuhusu Kanuni za Maadili na Mwenendo wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi

> PSPTB imekuwa ikiendelea na usimamizi madhubuti wa kanuni hizi. Kwa mfano, katika mwaka huu wa fedha 2025/2026, PSPTB imefanikiwa kusimamia mashauri ya wataalamu 15 ambao walikuwa na changamoto mbalimbali baada ya kufanyika uchunguzi na ukaguzi wa kina.

> Uelimishaji wananchi kuhusu Kanuni za Maadili na Mwenendo wa PSPTB sio tu wajibu wa PSPTB, bali ni fursa ya kujenga Tanzania yenye uwazi na haki. PSPTB, serikali na wananchi wote tuungane ili kanuni hizi zisiwe tu kwenye maandishi, bali zitekelezwe kila siku...

Katika ulimwengu wa siku hizi, ambapo ununuzi na ugavi wa umma unachukua nafasi kubwa katika maendeleo ya taifa, kanuni za maadili zinakuwa msingi wa kuhakikisha uwazi, haki na ufanisi. Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board - PSPTB) nchini Tanzania imetoa Kanuni za Maadili na Mwenendo wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, 2009, ambazo ni mwongozo wa kina kwa wataalamu waliosajiliwa. Hata hivyo, ili kanuni hizi ziwe na athari kubwa, ni muhimu kuwapa elimu wananchi wote si wataalamu pekee kuhusu umuhimu wake. Makala hii inachambua sababu za uelimishaji huu na faida zake.

**Uhusiano wa Kanuni za Maadili na Bodi ya PSPTB**

Ili kuelewa vizuri Kanuni za Maadili na Mwenendo wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, ni lazima tufahamu uhusiano wake na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB). Kama inavyoelezwa katika Sheria ya PSPTB, kifungu cha 4 kimeanzisha PSPTB kama taasisi rasmi inayosimamia taaluma ya ununuzi na ugavi nchini Tanzania.

Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa kifungu cha 7(d) cha sheria hiyo hiyo, PSPTB ina mamlaka kamili ya kusimamia maadili na mwenendo wa wataalamu waliosajiliwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Hii inahakikisha kuwa wataalamu wanazingatia viwango vya juu vya uadilifu, uwajibikaji na haki katika shughuli za ununuzi wa umma na binafsi.

Pamoja na sheria hii inayounda msingi wa PSPTB, kuna kanuni nyingine zinazoeleza mambo mbalimbali yanayohusiana na taaluma hii. Moja ya kanuni muhimu ni Kanuni za Maadili na Mwenendo wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, 2009, ambazo zinatoa mwongozo wa kina kuhusu jinsi wataalamu wanavyopaswa kufanya kazi bila migogoro ya maslahi, rushwa au ubaguzi.

PSPTB imekuwa ikiendelea na usimamizi madhubuti wa kanuni hizi. Kwa mfano, katika mwaka huu wa fedha 2025/2026, PSPTB imefanikiwa kusimamia mashauri ya wataalamu 15 ambao walikuwa na changamoto mbalimbali baada ya kufanyika uchunguzi na ukaguzi wa kina. Hii inaonyesha jitihada za bodi katika kudumisha nidhamu na kuwawajibisha wataalamu, hivyo kuimarisha uwazi na ufanisi katika sekta ya ununuzi na ugavi.

Kwa kuelewa uhusiano huu, wananchi na wadau wote wanaweza kushiriki kikamilifu katika kuripoti ukiukaji na kukuza utamaduni wa maadili. Hii itasaidia kujenga Tanzania yenye ufisadi mdogo na maendeleo endelevu.

**Kanuni za PSPTB ni Nini na Kwa Nini Zipo?**

Kanuni hizi, zilizoanza kutumika rasmi mwaka 2009, zinatumika kwa wataalamu wa ununuzi na ugavi waliosajiliwa chini ya PSPTB ambao wanafanya kazi upande wa sekta za umma na binafsi. Zinajumuisha kanuni za msingi kama uadilifu (integrity), uwajibikaji (accountability), haki (fairness), weledi (Professionalism), na usiri (confidentiality). Wataalamu wanatakiwa kuepuka migogoro ya maslahi, rushwa, ubaguzi na ulaghai, huku wakidumisha rekodi sahihi na kuzingatia sheria za



*Wakili Piencia Kiure, Mkuu wa Kitengo Cha Huduma za Kisheria*

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikwemo sheria ununuzi wa umma (Public Procurement Act).

Kwa mfano, kanuni inakataza kukubali zawadi zenye thamani zaidi ya Shilingi 50,000 bila tamko rasmi, na inawahimiza wananchi, wataalamu wa ununuzi na ugavi au yoyote kuripoti makosa ya uvunjwaji wa kanuni hizi. Pia kanuni hizi zinakataza wataalamu kujihusisha au kufanya vitendo vya kijanai au maswala yoyote yanayochafua taswira ya taaluma wakiwa kazini au nje ya kazi. Pia Ukiukaji unaweza kusababisha hatua za kinidhamu kama kufutwa usajili, kushushwa dalaja la usajili, onyo kali au kusimamishwa usajili. Hii inasaidia kuzuia ufisadi ambao umegharimu taifa mabilioni ya fedha katika miradi ya umma.

**Kwa Nini Tuwaelimishe Wananchi Kuhusu Kanuni Hizi?**

Watu wengi huona kanuni hizi ni za wataalamu wa ununuzi na ugavi pekee, lakini ukweli ni kwamba zinawahusu wananchi wote. Hapa kuna sababu kuu:

1. *Kuzuia Ufisadi na Kuhakikisha Thamani ya Pesa za Umma:* Wananchi wana haki ya kujua kuwa ununuzi wa dawa hospitalini, ujenzi wa barabara au vifaa vya shule unafanyika kwa haki. Elimu itawafaa wananchi kuripoti rushwa au upendeleo, hivyo kuimarisha imani katika serikali.
2. *Kuwapa Uwezo Wadau Wengine:* Wafanyabiashara, wakandarasi na wasambazaji wanahitaji kujua kanuni ili wasiingie mtegoni bila kujua. Kwa mfano, kutoa zawadi kwa afisa ununuzi kunaweza kuonekana kama rushwa, na kusababisha kutochaguliwa zabuni.
3. *Kukuza Utamaduni wa Maadili Katika Jamii:* Tanzania inakabiliwa na changamoto za ufisadi. Uelimishaji utawafundisha vijana, wafanyakazi na wazazi kuhusu uadilifu, hivyo kuwafaa hata katika maisha ya kila siku.
4. *Kusaidia Wataalamu Wenyewe:* Wakati wananchi wanapojua kanuni, wataalamu wataepuka shinikizo la kifisadi au migogoro, hivyo kuimarisha taaluma yao.

**Faida za Uelimishaji wa Umma**

1. *Kuongezeka kwa Uwazi:* Miradi ya umma itakuwa na ufanisi zaidi, na fedha za walipa kodi zitatumika vizuri.
2. *Kupungua kwa Kesi za Ufisadi*: Wananchi wakiwa na elimu, wataripoti mapema kwa mujibu wa sheria, hivyo kuzuia hasara kubwa.
3. *Maendeleo Endelevu:* Ununuzi wenye maadili utahakikisha bidhaa na huduma bora, kama dawa halisi au barabara za kudumu.
4. *Kuwapa Uwezo Wanawake na Vikundi Maalum:* Kanuni zinasisitiza usawa, hivyo elimu itawasaidia vikundi hivi kushiriki zabuni bila ubaguzi.

**Hitimisho: Wakati wa Kuchukua Hatua**

Uelimishaji wa wananchi kuhusu Kanuni za Maadili na Mwenendo wa PSPTB sio tu wajibu wa PSPTB, bali ni fursa ya kujenga Tanzania yenye uwazi na haki.PSPTB, serikali na wananchi wote tuungane ili kanuni hizi zisiwe tu maandishi, bali zitekelezwe kila siku. Tuanzishe leo – kwa maendeleo ya taifa letu!

Makala hii imeandikwa kwa lengo la kuelimisha. Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti rasmi ya PSPTB au wasiliana nao moja kwa moja.

## OZONE INTERNATIONAL

### Our Services

Prescriptive insights powered by the community. Powered by $2T of anonymized spend data and artificial intelligence, the targeted prescriptions leverage the wisdom of the extensive community to help your company capture significantly more measurable value than any other business spend management application on the market and drive strategic outcomes

### Why working with us?

## OZONE ZANZIBAR

Deployment times vary by complexity of the business; however, we will work with your team and implementation partner to go-live on agreed upon timeline

Tel: +255 777 889 988 or Tel: +255 774 004 400

Email. info@ozonezanzibar.com

Address. Michenzani Mall 3rd floor right door,

P.O. Box 538

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

## eGA

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019. Ni taasisi yenye jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi za umma.

eGA ni taasisi iliyoirithi Wakala ya Serikali Mtandao iliyoundwa Aprili 2012 kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 Sura ya 245 ya mwaka 1997 yenye jukumu na Mamlaka ya Kuratibu, Kusimamia na Kukuza Jitihada za Serikali Mtandao nchini Tanzania.

Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma, imesanifu, kujenga na kusimamia mifumo na miundombinu mbalimbali ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa umma. Huduma zetu zimesanifiwa na kutengenezwa na watalamu wa ndani kwa lengo la kuandaa mazingira wezeshi kwa taasisi za umma kuweza kutoa huduma bora kupitia miundombinu salama na mifumo shirikishi ya pamoja.

DYNATECH SOLUTIONS
Canon Partner

## DYNATECH SOLUTION LTD

Ni kampuni inayoongoza nchini Tanzania katika usambazaji wa Vifaa vya Tehama, Ikitoa ufumbuzi kamili wa kiteknolojia kwa sekta za Umma, Binafsi na Sekta za Kibenki, Ikijikita katika usambazaji wa vifaa muhimu kama vile kompyqqq uta za mezani na mkononi, mitandao ya LAN, na suluhisho za usalama wa Mifumo. Kwa lengo la kuwa mshirika anayeaminika zaidi nchini. Dynatech inajivunia ushirikiano wake uliothibitishwa na wazalishaji wakuu wa kimataifa kama HP, Canon, Dell, Sophos, Oracle na hivi karibuni imeongeza heshima ya kutambulika na Kutunukiwa tuzo kama Mshirika Bora wa Afrika Mashariki na Kati, Aliyethibitishwa na Canon. Utambulisho huu mpya na ushirikiano huu huimarisha ahadi ya Dynatech ya kutoa bidhaa halisi, usaidizi wa kiufundi wenye viwango vya kimataifa, na teknolojia bora kwa soko la Tanzania.

Dynatech Solutions Limited tunapatikanikana Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar

Bravado Group
*Inspiring Growth*

## BRAVADO

### OUR SERVICES



**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF FINANCE**

# PROCUREMENT AND SUPPLIES PROFESSIONALS AND TECHNICIANS BOARD (PSPTB)

## MINIMUM ENTRY QUALIFICATION FOR PROCUREMENT AND SUPPLY PRROFESSIONAL EXAMINATIONS

| LEVEL | QUALIFICATION |
|---|---|
| Professional (CPSP) Diploma I | a) Basic storekeeping or basic certificate issued by the Board.<br>b) Certificate (NTA 4) in either procurement and supply programs, procurement and logistics programs, procurement and supply management or transport and logistic programmes.<br>c) Ordinary Diploma (NTA 6) other than procurement and supply programmes or transport and logistic programs.<br>d) Certificate of competence for basic certificate in procurement and supply programs issued by the Board.<br>e) Any other professional qualifications recognized by the Board as equivalent to certificate in procurement and supply programs. |
| Professional (CPSP) Diploma II | Professional Diploma I or Foundation stage I issued by the Board |
| Graduate Professional I | a) Professional Diploma in Procurement and Supply programs or Procurement and Supply Management Foundation Certificate issued by the Board.<br>b) Ordinary Diploma (NTA 6) in Procurement and Supply programs or Procurement and Logistics programs.<br>c) Bachelor Degree other than procurement and supply programmes.<br>d) Certificate of competence in Professional Diploma for Procurement and Supply programs issued by the Board.<br>e) Any other professional qualifications recognized by the Board as equivalent to Professional Diploma in Procurement and Supply programs. |

| LEVEL | QUALIFICATION |
|---|---|
| Graduate Professional II | Professional Stage I or Graduate Professional I |
| Graduate Professional III | Professional Stage II or Graduate Professional II |
| Certified Procurement and Supply Professional (CPSP I) | a) Graduate Professional Certificate in Procurement and Supply management or Professional and Supply management or Professional III issued by the Board.<br>b) Bachelor Degree or (NTA 8) in Procurement and supply programs, Procurement and Logistics Management and Procurement and Supply Management.<br>c) Certified of competence for Graduate Professional in Procurement and Supply Management programs issued by the Board.<br>d) Any other professional qualifications recognized by the Board as equivalent to Graduate Professional Certificate in Procurement and Supply programmes. |
| Certified Procurement and Supply Professional (CPSP II) | Certified Professional I |

## Exemption Criteria

a) The Board accept and grant exemptions to holders of qualifications from other discipline on none core subject for curricula bearing five years at a time of the exemption application from any recognized institutions.

b) Candidates holding Master degree or PhD will NOT be required to conduct research paper, instead they shall be obliged to write independent professional practice project paper as shall be guided by the Board. Applicants bearing exemptions are those possessing masters or PhD during the admission at Certified Procurement Level one (CPSP I) examinations.

## FEE STRUCTURE FOR PROFESSIONAL EXAMINATIONS

New Candidacy registration fee – TZS 70,000
CPSP Research Workshop 400,000.00
CPSP Research/independent Paper process 360,000.00

## FEE STRUCTURE FOR PROFESSIONAL DIPLOMA BLOC

| | CODE | CORE SUBJECTS | NEW LEVEL FEE | NEW FEE PER SUBJECT | EXEMPTION FEE PER SUPPORTING SUBJECT | REFERRAL PER SUBJECT |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Professional Diploma I | D01 | Warehouse Operations | 175,000 | 35,000 | 40,000 | 40,000 |
| | D02 | Business Communication and Report Writing | | 35,000 | | 40,000 |
| | D03 | Business Mathematics and Statistics | | 35,000 | | 40,000 |
| | D04 | Information and Communication Technology | | 35,000 | | 40,000 |
| | D05 | Procurement Principles | | 35,000 | | 40.000 |
| | | | | **175,000** | | **200,000** |
| Professional Diploma II | D06 | Inventory Control | 210,000 | 35,000 | 40,000 | 40,000 |
| | D07 | Fundamentals of Procurement Contract Management | | 35,000 | | 40,000 |
| | D08 | Principles of Office Records Management | | 35,000 | | 40,000 |
| | D09 | Principles of Assets Management | | 35,000 | | 40,000 |
| | D10 | Tendering Process and Techniques | | 35,000 | | 40,000 |
| | D11 | Entrepreneurship and Commercial Knowledge | | 35,000 | | 40,000 |
| | | | | **210,000** | | **240,000** |

## FEE STRUCTURE FOR GRADUATE PROFESSIONAL BLOC

| | CODE | CORE SUBJECTS | NEW LEVEL FEE | NEW FEE PER SUBJECT | EXEMPTION FEE PER SUPPORTING SUBJECT | REFERRAL PER SUBJECT |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Graduate Professional I | G01 | Procurement Management | 250,000 | 50,000 | 80,000 | 50,000 |
| | G02 | Principles of Economics | | 50,000 | | 50,000 |
| | G03 | Principles and Practices of Management | | 50,000 | | 50,000 |
| | G04 | Legal Aspects of Procurement | | 50,000 | | 50,000 |
| | G05 | Warehouse Management | | 50,000 | | 50,000 |
| | | | | **250,000** | | **250,000** |
| Graduate Professional II | G06 | Public Procurement Management | 275,000 | 55,000 | 90,000 | 60,000 |
| | G07 | Decision Making Techniques | | 55,000 | | 60,000 |
| | G08 | Business Ethics and Professionalism | | 55,000 | | 60,000 |
| | G09 | Business Consulting Skills | | 55,000 | | 60,000 |
| | G10 | Asset Management | | 55,000 | | 60,000 |
| | | | | **275,000** | | **300,000** |
| Graduate Professional III | G11 | Financial Management | 300,000 | 60,000 | 100,000 | 70,000 |
| | G12 | Business Research Methods | | 60,000 | | 70,000 |
| | G13 | Inventory Management | | 60,000 | | 70,000 |
| | G14 | Supply Chain Planning | | 60,000 | | 70,000 |
| | G15 | Essentials of Procurement & Supply Chain Audit | | 60,000 | | 70,000 |
| | | | | **300,000** | | **350,000** |

## FEE STRUCTURE FOR CERTIFIED PROCUREMENT AND SUPPLY PROFESSIONAL (CPSP) BLOC

| | CODE | CORE SUBJECTS | NEW LEVEL FEE | NEW FEE PER SUBJECT | EXEMPTION FEE PER SUPPORTING SUBJECT | REFERRAL PER SUBJECT |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Certified Procurement and Supply Professional (CPSP I) | C01 | Fleet and Logistics Management | 390,000 | 65,000 | NOT EXEMPTED | 80,000 |
| | C02 | Consultancy and Entrepreneurship | | 65,000 | | 80,000 |
| | C03 | Strategic Supply Chain Management | | 65,000 | | 80,000 |
| | C04 | Project Management | | 65,000 | | 80,000 |
| | C05 | Business Negotiation | | 65,000 | | 80,000 |
| | C06 | Procurement Contract Management | | 65,000 | | 80,000 |
| | | | | **390,000** | | **480,000** |
| Certified Procurement and Supply Professional (CPSP II) | C07 | Managing Supply Chain Risks | 350 000 | 70,000 | NOT EXEMPTED | 90,000 |
| | C08 | Global Strategic Procurement | | 70,000 | | 90,000 |
| | C09 | Leadership and Governance | | 70,000 | | 90,000 |
| | C10 | Strategic Asset Management | | 70,000 | | 90,000 |
| | C11 | Procurement and Supply Chain Audit | | 70,000 | | 90,000 |
| | | | | **350,000** | | **450,000** |

**Main Office**
Executive Director
PSPTB
P.O.BOX 2663, Postcode 41108
DODOMA
7th Floor, Mkandarasi Place
Email: barua@psptb.go.tz

**Customer Service**
0738 441 971 – Usajili wa kitaaluma
0738 441 972 – Mitihani
0737 157 312 – Uhasibu
0737 622 477 – TEHEMA

# PROCUREMENT AND SUPPLY AUDITOR'S TRAINING PROGRAM: AUDITING SKILLS AND METHODOLOGY

## Introduction

The Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board (PSPTB) as a Professional regulator is mandated to train, register and regulate the conduct of procurement and supply auditors in Tanzania. In that regard, PSPTB has developed a professional training program in auditing skills and methodology for Procurement and supply auditors to enhance professionalism and professional practices in auditing procurement and supply chain management.

## Program Objectives

The training program for Procurement and Supply Auditors is intended to provide participants with a thorough understanding of practical aspects of procurement and supply audit, particularly, how it fits into an overall audit and functional review strategy. It will equip trainees with auditing knowledge and skills in line with the professional code of ethics and standards.

Equally, trained professionals who will complete the program will attempt qualifying examination for each module covered and will be eligible for an award of a Professional Competence Certificate in either Approved or Authorized Category in auditing skills and methodology.

## Who Should Attend?

This course is ideal for procurement and supply professionals executing and overseeing procurement and supply processes. It will equip the trainees into best practices and methodologies for conducting effective audits in the procurement and supply areas.

The program specifically designed to suit all practitioners registered under the Approved and Authorized category as per PSPTB Membership Registration Criteria who are responsible for Auditing Procurement and Supply processes, stock verification, and asset management in both the public and private sector.

## Training Modules

The designed modules focus on the introduction of Procurement and Supply for Auditing perspective, procurement and supply audit scope, conducting procurement and supply audit, risk assessment, ethical consideration, compliance to regulatory frameworks and Audit report writing as indicated in Table 1:

**TABLE 1: Learning module for Procurement and Supply Training Program**

| Categories | Module Name |
|---|---|
| Approved and Authorized Category Program | Procurement and Supply chain management for Auditing Perspective |
| | Risk-based Procurement and Supply Chain Auditing and Investigation |
| | Legal framework and standards for professional practice in auditing |
| | Leadership and governance |
| | Report writing and Documentation in auditing and investigation. |

## How to apply?

Applicants are encouraged to apply for this training by clicking a link on online event registration found on the PSPTB website http://www.psptb.go.tz or clicking direct the http://registration.psptb.go.tz Upon registration applicant will receive a control number for processing payment.

## location and Dates:

The First Cohort program is intended to be conducted in Arusha and Dar es Salaam;

(a) Part Time (Evening) Training Program from 02nd to 28th September 2024 - DSM

(b) Full Time (Executive) Training Program from 16th to 28th September 2024- ARUSHA

## Participation Fees and training duration

The program has been designed in five modules which are intended to be conducted on the basis of full-time (Executive Training program or part-time (Evening) Training program its fees indicated below;

(a) **Full-time (executive) training program**

The Approved fee for a full-time (executive) Training program is **TZS 520,000/=** per module; Maximum training duration three (6) days per module.

(b) **Part - Time (evening) training program**

The approved fees for a part-time (evening) training program is **TZS 400,000/=** per module: Maximum Training Duration six (6) days per module.

## Communication and confirmation

Please **confirm** your attendance and payment earlier **before** or **on 30th August 2024**. For any inquiry, please, do not hesitate to call 0738441972 during office hours.

**Issued by:**

**Godfred B. Mbanyi**


**EXECUTIVE DIRECTOR**


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi
psptb
PONGEZI
Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hasaan
Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) tunakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.** Tunakuombea kheri katika utekelezaji wa majukumu yako. PSPTB inakuahidi ushirikiano katika kuleta maendeleo chanya ya nchi yetu
PSPTB TV Bodi Ununuzi psptbofficial www.psptb.go.tz


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi
psptb
PONGEZI
Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi
Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) tunakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.** Tunakuombea kheri katika utekelezaji wa majukumu yako. PSPTB inakuahidi ushirikiano katika kuleta maendeleo chanya ya nchi yetu
PSPTB TV Bodi Ununuzi psptbofficial www.psptb.go.tz



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi
psptb
PONGEZI
Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba
Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) tunakupongeza kwa kuteuliwa kuwa **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.** Tunakuombea kheri katika utekelezaji wa majukumu yako. PSPTB inakuahidi ushirikiano katika kuleta maendeleo chanya ya nchi yetu
PSPTB TV Bodi Ununuzi psptbofficial www.psptb.go.tz


# Salamu za Pongezi












# WADHAMINI WAKONGAMANO LA MWAKA LA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI


**Jarida hili hutolewa na:**
Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB)
Ghorofa ya 7, Mkandarasi Place
S.L.P. 2663, Postcode 41108, Dodoma
Simu: +255 628 903 820

**Nyerere Road, GPSA Premises**
S.L.P. 5993, Dar es Salaam / Simu: +255 22 286 5860

**barua@psptb.go.tz / www.psptb.go.tz psptbofficial Bodi Ununuzi PSPTB TV**